BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KATIKA UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE (SFNA) 2019

## 01 KISWAHILI

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KATIKA UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE (SFNA) 2019

# 01 KISWAHILI

*Kimechapishwa na*
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P. 2624,
Dar es Salaam, Tanzania.

© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2020

Haki zote zimehifadhiwa.

## YALIYOMO


1.0 UTANGULIZI ........................................................................ 1

2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI ........................................ 1

2.1 Sehemu A ........................................................................ 2

2.2 Sehemu B ........................................................................ 7

2.3 Sehemu C ........................................................................ 12

2.4 Sehemu D ........................................................................ 17

2.5 Sehemu E ........................................................................ 24

3.0 UCHAMBUZI WA KUFAULU KWA WANAFUNZI KATIKA MAHIRI MBALIMBALI ........................................................................ 31

4.0 HITIMISHO ........................................................................ 32

5.0 MAONI NA MAPENDEKEZO ........................................................................ 32

KIAMBATISHO NA I ........................................................................ 34

KIAMBATISHO NA 2 ........................................................................ 35

## DIBAJI

Baraza la Mitihani la Tanzania limeandaa taarifa ya uchambuzi wa majibu ya wanafunzi katika Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne kwa somo la Kiswahili mwaka 2019.Taarifa hii inachambua majibu ya maswali ya Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne kwa somo la Kiswahili mwaka 2019. Lengo la taarifa hii ni kutoa mrejesho kwa walimu, wanafunzi, watunga sera, wathibiti ubora wa elimu, watunga mitaala na wadau wengine wa elimu. Aidha, taarifa hii inaonesha jinsi mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji ulivyomwezesha au kushindwa kumwezesha mwanafunzi kupata maarifa stahiki kwa kipindi cha miaka minne ya elimu ya msingi.

Pamoja na hayo, taarifa hii imechambua sababu mbalimbali zilizochangia baadhi ya wanafunzi kushindwa kujibu maswali kwa ufasaha. Baadhi ya sababu hizo ni kushindwa kutambua matakwa ya swali, kukosa maarifa na athari ya lugha mama. Mtawanyiko wa majibu ya wanafunzi kwa kila swali umeainishwa katika uchambuzi huu kwa kutumia vielelezo, chati na maelezo.

Baraza la Mitihani la Tanzania linatarajia kuwa, taarifa hii itawawezesha wanafunzi na wasimamizi wa elimu kubuni mbinu zitakazosaidia kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili ili kukabiliana na changamoto zilizobainishwa katika taarifa hii. Aidha, Baraza la Mitihani la Tanzania linaamini kuwa, maoni yaliyotolewa yakifanyiwa kazi, yatasaidia kuongeza umahiri wa wanafunzi na hatimaye kuimarisha ubora wa elimu inayotolewa nchini.

Mwisho, Baraza la Mitihani la Tanzania linatoa shukrani za dhati kwa wote walioshiriki kuandaa taarifa hii wakiwemo Maafisa Mitihani, Wataalam wa

TEHAMA na wataalam wengine wa elimu walioshiriki katika kuandaa uchambuzi huu.

Dkt. Charles E. Msonde

**KATIBU MTENDAJI**

## 1.0 UTANGULIZI

Taarifa hii imeandaliwa kwa lengo la kutoa mrejesho wa namna ambavyo wanafunzi walijibu maswali ya upimaji wa somo la Kiswahili mwezi Novemba 2019. Upimaji huu ni wa pili katika mtaala mpya unaozingatia ujenzi wa umahiri kwa mwanafunzi katika stadi ya kuzungumza, kusikiliza, kusoma na kuandika. Upimaji wa somo la Kiswahili ulikuwa na sehemu tano ambazo ni A. *Uwezo wa mwanafunzi katika kusikiliza matamshi ya silabi, maneno na sentensi na kuyaandika (Imla).* B. *Umahiri wa mwanafunzi wa kubadili majina kuwa vitendo katika mawasiliano.* C. *Umahiri wa mwanafunzi kutumia methali na vitendawili katika mawasiliano mbalimbali.* D. *Uwezo wa mwanafunzi wa kuandika barua ya kirafiki* na E. *Uwezo wa mwanafunzi katika kusoma kwa ufasaha na kuonesha uelewa wa matini (shairi)* aliyolisoma. Sehemu hizo tano zimetoka katika umahiri mkuu ambao ni *kuwasiliana katika miktadha mbalimbali* na *kuonesha uelewa wa jambo alilolisikiliza au kulisoma*. Kila sehemu ilikuwa na swali **moja (1)** lenye vipengele **vitano (5)** vyenye jumla ya alama kumi (10). Jumla ya wanafunzi **1,786,729** walisajiliwa kufanya Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne na waliopimwa katika somo la Kiswahili walikuwa **1,664,019** Aidha, wanafunzi **1,475,263** sawa na asilimia **88.67** ndiyo waliofaulu katika upimaji huo.

## 2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI

Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi umefanyika kwa kuainisha maswali yote ya Upimaji wa Darasa la Nne na majibu waliyoandika na wanafunzi kwa kuzingatia maelekezo yaliyotolewa kwa kila sehemu. Idadi na asilimia ya wanafunzi walioweza na walioshindwa kuandika jibu sahihi imewasilishwa katika chati na vielelezo. Uchambuzi wa

sababu zilizochangia wanafunzi kujibu au kushindwa kujibu maswali kwa usahihi zimeainishwa.

## 2.1 Sehemu A

Sehemu hii ilikuwa na swali moja la imla na mwanafunzi alitakiwa kusikiliza kwa makini sentensi tano (5) alizosomewa, kisha kuziandika kwa usahihi. Kila sentensi ilikuwa na maneno manne yenye nusu alama kwa kila neno na kila sentensi ilikuwa na alama 2, hivyo kufanya jumla ya alama kumi (10). Swali lilitoka kwenye umahiri mkuu wa kuwasiliana katika miktatha mbalimbali. Swali lililenga kupima uelewa wa mwanafunzi katika kuandika sentensi kwa kuzingatia alama za uandishi na kutambua sauti mbalimbali katika matamshi ya silabi, maneno na sentensi.

**Swali la 1**:**Sikiliza kwa makini sentensi zinazosomwa kisha uziandike kwa usahihi** katika nafasi zilizoachwa wazi.

(i) ____________________________________________

(ii) ____________________________________________

(iii) ____________________________________________

(iv) ____________________________________________

(v) ____________________________________________

Zifuatazo ni sentensi walizosomewa wanafunzi:

(i) Nywele zetu zimependeza sana.


(ii) Tunapaswa kutunza bustani vizuri.

(iii) Mchwa walikula mazao shambani.

(iv) Usithubutu kuiba ni dhambi.

(v) Mwindaji hodari alipewa pongezi.


Swali hili lilijibiwa na wanafunzi 1,664,019 (100%). Kiwango cha kufaulu katika swali kilikuwa kizuri ambapo jumla ya wanafunzi 651,481 (39.2%) waliweza kujibu vizuri sana vipengele vyote 5 na kupata alama 10. Aidha wanafunzi 657,999 (37.8%) walifanya vizuri na kupata alama kuanzia 6.5 hadi 9.5. Wanafunzi 132,931 (8.0%) walipata alama za wastani kuanzia 3 hadi 6. Vilevile wanafunzi 221,608 (13.3%) walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 2.5. **Chati Na. 1.** inaonesha viwango vya kufaulu vya wanafunzi kwa asilimia.




**Chati Na. 1:** *Asilimia ya ufaulu kwa wanafunzi katika swali la 1*.

Uchambuzi unaonesha kuwa, wanafunzi 1,442,411 (86.7%) walifaulu vizuri swali hili. Kati yao, wanafunzi 651,481 (39.2%) walifaulu kwa kiwango kizuri sana kwa kupata alama zote. Wanafunzi hao walikuwa na maarifa ya kusoma na kuandika, hivyo kuweza kubaini sauti zinazounda maneno yaliyosomwa na kuyaandika kwa usahihi huku wakizingatia alama za uandishi pamoja na kutumia herufi kubwa mwanzoni mwa sentensi.

Aidha, wanafunzi hao walikuwa na weledi wa kubaini na kuandika sauti zenye silabi mwambatano zenye mfuatano wa konsonanti kwa usahihi kama vile maneno *nywele* (nyw), *tunapaswa* (sw), *mchwa* (chw), *usithubutu* (th) na *mwindaji* (mw). Maneno yenye silabi hizo yalikuwa katika sentensi za imla walizosomewa. Kwa ujumla, wanafunzi hao walikuwa na umahiri wa kusikiliza na kubaini sauti zinazounda maneno, matamshi ya herufi yanayounda maneno pamoja na kuandika alama za uandishi kwa usahihi. Kielelezo 1.1 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyejibu kwa usahihi vipengele vitano (5) vya swali hili.



1. **Sikiliza kwa makini sentensi zinazosomwa kisha uziandike kwa usahihi** katika nafasi zilizoachwa wazi.

(i) Nywele zetu zimependeza sana.

(ii) Tunapaswa kufunza bustani vizuri.

(iii) Mchwa walikula mazao shambani.

(iv) Usithubutu kuiba ni dhambi.


(v) Mwindaji hodari alipewa pongezi.

Kielelezo 1.1: *Jibu sahihi la mwanafunzi katika swali la 1*.

Kielelezo 1.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mwanafunzi ambaye aliweza kuandika kwa usahihi sentensi zote tano kwa kuzingatia alama za uandishi na herufi kubwa na ndogo na kupata alama zote.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, wanafunzi 132,931 (8.0%) walipata alama za wastani kuanzia 3 hadi 6. Hawa waliweza kuandika kwa usahihi maneno 6 hadi 12 katika sentensi zote tano na kupata alama kuanzia 3 hadi 6. Wanafunzi hao walikuwa na maarifa ya matumizi ya alama za uandishi ingawa walishindwa kuandika baadhi ya maneno

yenye silabi mwambatano pamoja na kutozingatia alama za uandishi. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja alichanganya matamshi ya herufi *l* na *r* kwenye neno “Nywele” na kuandika *Nyere*. Vilevile alichanganya herufi kubwa na ndogo kwenye maneno yake. Kwa mfano, kwenye baadhi ya maneno kwenye kipengele (i) na neno la kwanza (ii). Aidha, alishindwa kuandika kwa usahihi maneno kama vile “Usithubutu” na kuandika *Husisubu* katika kipengele (iv) pamoja na neno “Mwindaji” na aliandika *Wihindaji* kipengele cha (v). Kielelezo 1.2 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyepata alama za wastani.


1. **Sikiliza kwa makini sentensi zinazosomwa kisha uziandike kwa usahihi** katika nafasi zilizoachwa wazi.

(i) Nyere zetu zime pendeza sana

(ii) Tuna Pasiwa kutu bustani vizuri

(iii) Mchwa walikula mazao shambani

(iv) Husisubu kuiba ni dhambi


(v) Wihindaji hodari alipewa pongezwa

Kielelezo 1.2: *Jibu la wastani la mwanafunzi katika swali la 2*.

Kielelezo 1.2 kinaonesha majibu ya mwanafunzi aliyeweza kuandika baadhi ya maneno kwa usahihi na kushindwa kuandika maneno yenye silabi mwambatano pamoja na kutozingatia kanuni za uandishi hivyo kumfanya kupata alama za wastani.

Hata hivyo, wanafunzi 221,608 (13.3%) walikuwa na kiwango hafifu cha ufaulu kwa kuwa walishindwa kuandika kwa usahihi maneno mengi katika sentensi zote na kupata alama kuanzia 0 hadi 2.5. Wanafunzi hao walishindwa kuandika kwa usahihi sauti za herufi za silabi ambazo huunda maneno ili kuunda sentensi. Aidha, baadhi ya

wanafunzi hawakuwa na umahiri wa kusoma na kuandika na hivyo kushindwa kufuata misingi na taratibu za lugha ya Kiswahili hasa katika miundo ya silabi katika kuunda neno. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja alichanganya herufi ndogo na herufi kubwa katika maneno, vilevile alishindwa kuandika baadhi ya silabi sahihi katika maneno kama vile, neno “Usithubutu” aliandika *usisubuta,* “Mwindaji” aliandika *muindasi, neno “*pongezi” aliandika *pongezwa* na neno “Dhambi” aliandika *zambi*. Hivyo wanafunzi hao hawajui kuunda sauti za silabi mwambatano. Kielelezo 1.3 kinaonesha sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyejibu vibaya swali hili.


1. **Sikiliza kwa makini sentensi zinazosomwa kisha uziandike kwa usahihi** katika nafasi zilizoachwa wazi.

(i) nywele zetu zime pendezasa pa.

(ii) tunapaswa kutazwabostanivi zuli.

(iii) mchwa wali kula mazaashambani

(iv) usisubuta kuibani zambi.

(v) muindasi dali alipewapongezwa.

Kielelezo 1.3: *Jibu baya la mwanafunzi katika swali la 1*.

Kielelezo 1.3 kinaonesha majibu ya mwanafunzi ambaye aliandika silabi zisizo sahihi na kushindwa kuandika sauti za silabi mwambatano na ali changanya herufi kubwa na ndogo katika maneno kinyume na matakwa ya swali.


## 2.2 Sehemu B

Sehemu hii ilikuwa na swali moja lenye vipengele vitano (5) ambavyo vililenga kupima uundaji wa kubadili majina kuwa vitendo. Kila kipengele kilikuwa na alama 2 ambapo jumla ya alama katika swali hili ilikuwa 10. Swali lilitoka katika umahiri mkuu wa kuonesha uelewa wa jambo alilolisikiliza au kulisoma**.**

**Swali la 2**: Badili majina yafuatayo kuwa vitendo. Kipengele cha (i) kimetumika kama mfano.


(i) Mchezo Cheza.
(ii) Maombi ______________________
(iii) Pigo ______________________
(iv) Wimbo ______________________
(v) Wazo ______________________
(vi) Kilimo ______________________

Swali hili lilijibiwa na wanafunzi 1,664,019 (100%). Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa cha wastani. Jumla ya wanafunzi 388,768 (23.4%) waliweza kujibu vizuri sana vipengele vyote 5 na kupata alama 10. Aidha, wanafunzi 242,859 (14.6%) walijibu vizuri na kupata alama kuanzia 6.5 hadi 9.5. Wanafunzi 364,388 (21.9%) walipata alama za wastani kuanzia 3 hadi 6. Vilevile wanafunzi 668,004 (40.1%) walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 2.5 **Chati Na. 2.** inaonesha viwango vya kufaulu vya wanafunzi kwa asilimia.




**Chati Na. 2**: *Asilimia ya ufaulu kwa wanafunzi katika swali la 2*.

Uchambuzi unaonesha kuwa, wanafunzi 996,015 (59.9%) walikuwa na kiwango cha wastani cha ufaulu. Kati yao wanafunzi 668,004 (40.1%) walipata alama kuanzia 0 hadi 2.5 hii inaonesha kuwa, wanafunzi hao walishindwa kubadili majina kuwa vitendo. Lakini wapo waliochanganya dhana ya kubadili majina kuwa matendo na dhana ya kuunda maneno mapya kwa kudondosha herufi kutoka kwenye neno (majina) na kuunda maneno kama vile; "Maombi" kuwa ombi, Pigo kuwa igo, Wimbo kuwa imbo, Wazo kuwa azo na "Kilimo" kuwa limo. Maneno hayo yanaonesha wanafunzi walifanya udondoshaji wa herufi za mwanzoni za majina kinyume na matakwa ya swali. Aidha, Wapo wanafunzi walioandika wingi wa majina kwenye nafasi ya kuandika vitendo. Hali hii inadhihirisha kuwa wanafunzi hao hawakuwa na uelewa kuhusu dhana ya kubadili majina kuwa vitendo. Kielelezo Na. 2.1 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kubadili majina kuwa vitendo.


2. Badili majina yafuatayo kuwa vitendo. Kipengele cha (i) kimetumika kama mfano.

(i) Mchezo Cheza

(ii) Maombi ombi

(iii) Pigo mapigo

(iv) Wimbo nyimbo

(v) Wazo mawazo

(vi) Kilimo vilimo

Kielelezo 2.1: *Jibu baya la mwanafunzi katika swali la 2*.

Kielelezo 2.1 kinaonesha majibu ya mwanafunzi aliyejibu kinyume na matakwa ya swali ambapo badala ya kubadili majina kuwa vitendo aliandika wingi wa majina aliyopewa.

Hata hivyo, wanafunzi 364,388 (21.9%) walipata alama za wastani kuanzia 3 hadi 6 na waliweza kujibu kwa usahihi maneno 2 hadi 3 katika swali husika. Wanafunzi hao waliweza kubadili baadhi ya majina kuwa vitendo kwa usahihi. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja katika (v) na (vi) aliandika wingi wa majina aliyopewa ambapo ni kinyume na matakwa ya swali. Vilevile, mwanafunzi huyu aliandika herufi ndogo mwanzoni mwa neno, hivyo kuweza kupata alama za wastani. Kielelezo Na. 2.2 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeweza kubadili baadhi ya majina kuwa vitendo.

2. Badili majina yafuatayo kuwa vitendo. Kipengele cha (i) kimetumika kama mfano.

(i) Mchezo Cheza

(ii) Maombi omba

(iii) Pigo piga

(iv) Wimbo imba

(v) Wazo mawazo

(vi) Kilimo vilimo

Kielelezo Na. 2.2: *Jibu la wastani la mwanafunzi katika swali la 2*.

Kielelezo 2.2 kinaonesha sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeweza kujibu kwa usahihi baadhi ya vipengele. Hata hivyo alishindwa katika vipengele vingine kutokana na kutoa majibu ambayo ni kinyume na matakwa ya swali.

Aidha, uchambuzi wa majibu ya wanafunzi unaonesha kuwa, wanafunzi 388,768 (23.4%) waliweza kubadili majina kuwa vitendo kwa usahihi na kupata alama zote 10. Hii inaonesha kuwa, wanafunzi waliojibu vizuri swali hili walikuwa na umahiri na maarifa ya kutosha kuhusu dhana ya kubadili majina kuwa vitendo na kuweza kubaini vitendo sahihi vinavyotokana na majina husika. Kielelezo.2.3 ni sampuli ya mwanafunzi aliyeweza kubadili majina kuwa vitendo kwa usahihi.

2. Badili majina yafuatayo kuwa vitendo. Kipengele cha (i) kimetumika kama mfano.

(i) Mchezo Cheza

(ii) Maombi Omba

(iii) Pigo Piga

(iv) Wimbo Imba

(v) Wazo Waza

(vi) Kilimo Lima

Kielelezo 2.3: *Jibu sahihi la mwanafunzi katika swali la 2*.

Kielelezo 2.3: kinaonesha sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyejibu vizuri kwa kufuata matakwa ya swali kwa kuweza kubadili majina kuwa vitendo huku akizingatia uhusiano uliopo kati ya majina hayo na vitendo vilivyoundwa.

## 2.3 Sehemu C

Sehemu hii ilikuwa na swali moja lenye vipengele vitano (5) na lilitoka katika umahiri wa kuwasiliana katika miktadha mbalimbali ambapo lilikuwa na jumla ya alama 10. Swali lililenga kupima ujuzi wa mwanafunzi kutumia methali na vitendawili katika miktadha mbalimbali.

**Swali la 3:** (i) Kamilisha methali ifuatayo "jungu kuu_______________

_____________________________________________"

(ii) Andika methali itakayotumika kumuonya mtu anayependa kuchagua sana vitu na hatimaye kupata kitu kibaya.____________________________________

_____________________________________________

(iii) Andika methali inayohimiza watu kufanya kazi kwa kushirikiana?___________________________________

_____________________________________________

(iv) "Msema kweli mpenzi wa mungu." Methali hii inafundisha nini?________________________________


_____________________________________________

(v) Tegua kitendawili kisemacho "Bibi hatui mzigo wake."

_______________________________________________


Swali hili lilijibiwa na wanafunzi 1,664,019 (100%). Kiwango cha ufaulu katika swali kilikuwa kizuri ambapo jumla ya wanafunzi 214,345 (12.9%) waliweza kujibu vizuri sana vipengele vyote 5 na kupata alama 10. Aidha wanafunzi 281,387 (16.9%) walifanya vizuri na kupata alama kuanzia 6.5 hadi 9.5. Wanafunzi 665,138 (40%) walipata alama za wastani kuanzia 3 hadi 6. Vilevile wanafunzi 503,149 (30.2%) walipata

alama hafifu kuanzia 0 hadi 2.5. **Chati Na. 3** inaonesha viwango vya kufaulu na asilimia ya wanafunzi.




**Chati Na: 3**: *Asilimia ya kufaulu kwa wanafunzi katika swali la 3*.

Uchambuzi unaonesha kuwa wanafunzi 1,160,870 (69.8%) walikuwa na kiwango kizuri cha ufaulu. Kati yao wanafunzi 214,345 (12.9%) walikuwa na kiwango kizuri sana cha kufaulu na kupata alama 10. Hawa waliweza kujibu kwa kufuata matakwa ya swali kwa kila kipengele, kukamilisha methali kwa usahihi, kutoa mafunzo yanayopatikana katika methali husika pamoja na kutegua vitendaliwi. Hivyo, wanafunzi hao walikuwa na weledi na maarifa ya kutosha ya kuwasiliana katika miktadha mbalimbali, hususani katika kutambua methali zinavyotumika na kuelezea maana zake pamoja na kutegua vitendawili. Kielelezo 3.1 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeweza kujibu vipengele vyote 5 vya swali kwa usahihi.



3. (i) Kamilisha methali ifuatayo "jungu kuu Halikosi ukoko. ____________________"

(ii) Andika methali itakayotumika kumuonya mtu anayependa kuchagua sana vitu na hatimaye kupata kitu kibaya. Mchagua nazi hupata koroma.

(iii) Andika methali inayohimiza watu kufanya kazi kwa kushirikiana?

Umoja ni nguvu utengano ni ~~uth~~ udhaifu.

(iv) "Msema kweli mpenzi wa Mungu." Methali hii inafundisha nini?

Inatufundisha kuwa mtu mkweli ni rafiki wa Mungu.

(v) Tegua kitendawili kisemacho "Bibi hatui mzigo wake."


Kobe/Konokono.

Kielelezo 3.1: *Jibu sahihi la mwanafunzi katika swali la 3.*

Kielelezo 3.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyejibu vizuri kwa kufuata matakwa ya swali ambapo aliweza kukamilisha methali kwa usahihi, kutoa mafunzo yanayopatikana katika methali husika pamoja na kutegua vitendawili.

Aidha, uchambuzi unaonesha kuwa, wanafunzi 665,138 sawa na asilimia 40 walipata alama za wastani kuanzia 3 hadi 6 kwa kuweza kujibu baadhi ya vipengele kwa kufuata matakwa ya swali. Aidha,

wanafunzi wengine walishindwa kukamilisha methali kwa usahihi, kutoa mafunzo yanayopatikana katika methali husika pamoja na kutegua vitendaliwi kutokana na kukosa maarifa ya kutambua methali na vitendawili zinavyotumika katika miktadha mbalimbali. Kielelezo 3.2 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyepata alama za wastani.


3. (i) Kamilisha methali ifuatayo "jungu kuu alikosi ukoko. ____________________"

(ii) Andika methali itakayotumika kumuonya mtu anayependa kuchagua sana vitu na hatimaye kupata kitu kibaya. Asiyefundwana mama ye ufunza na ulimwengu

(iii) Andika methali inayohimiza watu kufanya kazi kwa kushirikiana?

umojani nguvu utengano ni uvumilizu

(iv) "Msema kweli mpenzi wa Mungu." Methali hii inafundisha nini?

ndiye lafi wa kweli

(v) Tegua kitendawili kisemacho "Bibi hatui mzigo wake."

konokono

Kielelezo 3.2: *Jibu la wastani la wanafunzi katika swali la 3*.

Kielelezo 3.2 kinaonesha sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeweza kujibu kwa usahihi baadhi ya vipengele na kushindwa vipengele vingine kutokana na kutoa majibu yasiyokidhi matakwa ya swali.

Pia, wanafunzi 503,149 (30.2%) walikuwa na kiwango hafifu cha kufaulu na kupata alama kuanzia 0 hadi 2.5 kwa kukosa maarifa

kuhusu dhana ya methali na vitendawili. Kwa mfano, wakati katika kipengele (i) - (v) mwanafunzi alitakiwa kuandika jibu sahihi kulingana na matakwa ya swali kuhusu vitendawili na methali, aliandika vipengele vya barua ya kirafiki vilivyopo katika swali la 4 kama vile: *Madhumuni*, *S.L.P 100, Zawadi, 2021* na *13/11/2018*. Kwa ujumla, uchambuzi huu umebaini kuwa wanafunzi waliopata alama kuanzia 0 hadi 2.5 walikosa maarifa ya kutambua methali na vitendawili zinavyotumika katika miktadha mbalimbali, hususan katika kukamilisha methali husika, katika kuelewa mafunzo mbalimbali yanayopatikana katika methali na kutegua vitendawili. Kielelezo 3.1 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kujibu swali kwa usahihi.

3. (i) Kamilisha methali ifuatayo "jungu kuu S.L.P 100 ____________________"

(ii) Andika methali itakayotumika kumuonya mtu anayependa kuchagua sana vitu na hatimaye kupata kitu kibaya. 13\11\2018

(iii) Andika methali inayohimiza watu kufanya kazi kwa kushirikiana?

madhumuni

(iv) "Msema kweli mpenzi wa Mungu." Methali hii inafundisha nini?

2021

(v) Tegua kitendawili kisemacho "Bibi hatui mzigo wake."

zawadi

Kielelezo 3.3: *Jibu baya la mwanafunzi katika swali la 3*.

Kielelezo 3.3 kinaonesha sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyejibu vibaya swali kwa kuandika vipengele vya barua ya kirafiki badala ya kukamilisha methali kwa usahihi, kutoa mafunzo yanayopatikana katika methali husika pamoja na kutegua vitendaliwi.

## 2.4 Sehemu D

Sehemu hii ilikuwa na swali moja lenye vipengele vitano (5) ambapo kila kipengele kina alama 2 zinazofanya jumla ya alama 10. Swali lilitoka katika umahiri wa kuwasiliana katika miktadha mbalimbali na lililenga kupima ujuzi wa mwanafunzi katika kuunda barua ya kirafiki.

**Swali la 4:** Kamilisha nafasi zilizo wazi kwenye barua kwa kuchagua majibu sahihi uliyopewa kwenye kisanduku.

| | | |
|---|---|---|
| Madhumuni | S.L.P 100 | Zawadi |
| 2021 | 13/11/2018 | |

Shule ya Msingi Mwembe,

(i)________________

Songwe.

(ii)_______________.

Mpendwa mama, shikamoo.

Ni imani yangu kuwa unaendelea vizuri na shughuli za kilimo. Naamini pia ndugu zangu wengine hawajambo hapo nyumbani.

(iii) ___________________ ya barua hii ni kutaka kukujulisha kuwa nimefaulu Upimaji wa Kitaifa wa Darasa


la Nne tuliofanya mwishoni mwa mwaka jana. Nimefurahi sana kwa kuwa nimefaulu vizuri kwa kupata Daraja A. Ni matumaini yangu kuwa hata mdogo wangu Furaha atafaulu Upimaji wake wa Darasa la Nne wa mwaka (iv)_______________.

Ninakushukuru kwa kunihimiza kusoma kwa bidii. Kufaulu kwangu kumetokana na maneno yako ya hamasa.

Kwa leo sina mengi zaidi. Ninaomba uwasalimie wadogo zangu wote.

Ni mimi mwanao (v) ______________.

Swali hili lilijibiwa na wanafunzi 1,664,019 (100%). Kiwango cha kufaulu katika swali kilikuwa kizuri ambapo jumla ya wanafunzi 796,621 (47.9%) waliweza kujibu vizuri sana vipengele vyote 5 na kupata alama 10. Aidha, wanafunzi 117,020 (7.0%) walifanya vizuri na kupata alama 6.5 hadi 9.5. Wanafunzi 316,622 (19.0%) walipata alama za wastani kuanzia 3 hadi 6. Vilevile wanafunzi 433,756 (26.1%) walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 2.5 **Chati Na. 4** inaonesha viwango vya kufaulu vya wanafunzi kwa asilimia.




**Chati Na. 4**: *Asilimia ya ufaulu kwa wanafunzi katika swali la 4*.

Uchambuzi unaonesha kuwa wanafunzi 1,230,263 (73.9%) walikuwa na kiwango kizuri cha ufaulu ambapo wanafunzi 796,621 (47.9%) walifaulu kwa kiwango kizuri sana. Wanafunzi hao waliweza kukamilisha nafasi zilizo wazi kwenye barua kwa kuchagua majibu sahihi waliyopewa kwenye kisanduku kutokana na uelewa wao kuhusu muundo wa barua ya kirafiki. Wanafunzi hao waliweza kubaini sehemu sahihi ya kuweka *S.L.P* (i) na *tarehe* na (ii) ambavyo hukaa upande wa kulia wa barua. Aidha, waliweza kubaini kuwa neno *Madhumuni* (iii) hukaa mwanzoni mwa kiini cha barua. Vilevile, waliweza kutambua tarakimu *2021* (iv) kuwa ni mwaka sahihi kutokana na muktadha wa barua husika. Mwisho, wanafunzi hao waliweza kubaini neno sahihi katika (v) kuwa ni *Zawadi* kwa sababu ni jina la mwandishi wa barua ya kirafiki na hukaa mwishoni mwa barua. Kwa ujumla, wanafunzi walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu vipengele vya muundo wa barua ya kirafiki. Kielelezo Na. 4.1 ni sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeweza kukamilisha barua kwa usahihi.

4. Kamilisha nafasi zilizo wazi kwenye barua kwa kuchagua majibu sahihi uliyopewa kwenye kisanduku.

| | | |
|---|---|---|
| Madhumuni | S.L.P 100 | Zawadi |
| 2021 | 13/11/2018 | |

Shule ya Msingi Mwembe,

(i) S·L·P.100,

Songwe.

(ii) 13/11/2018

Mpendwa mama, shikamoo.

Ni imani yangu kuwa unaendelea vizuri na shughuli za kilimo. Naamini pia ndugu zangu wengine hawajambo hapo nyumbani.

(iii) Madhumuni ya barua hii ni kutaka kukujulisha kuwa nimefaulu Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne tuliofanya mwishoni mwa mwaka jana. Nimefurahi sana kwa kuwa nimefaulu vizuri kwa kupata Daraja A. Ni matumaini yangu hata mdogo wangu Furaha atafaulu Upimaji wake wa Darasa la Nne wa mwaka (iv) 2021.

Ninakushukuru kwa kunihimiza kusoma kwa bidii. Kufaulu kwangu kumetokana na maneno yako ya hamasa.

Kwa leo sina mengi zaidi. Ninaomba uwasalimie wadogo zangu wote.

Ni mimi mwanao (v) Zawadi.

Kielelezo 4.1: *Majibu mazuri ya mwanafunzi katika swali la 4.*

Kielelezo 4.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeweza kujibu kwa usahihi kwa kukamilisha nafasi zilizo wazi kwenye barua kwa kuchagua majibu sahihi aliyopewa kwenye kisanduku.

Aidha, uchambuzi unaonesha kuwa wanafunzi 316,622 (19.0%) walipata alama za wastani kuanzia 3 hadi 6. Waliweza kukamilisha nafasi zilizo wazi kwenye barua kwa kuchagua baadhi ya majibu sahihi waliyopewa kwenye kisanduku. Wanafunzi hawa walikuwa na maarifa ya kukamilisha barua japokuwa walichanganya baadhi ya vipengele na wengine kujaza herufi ya jibu kinyume na matakwa ya swali. Kielelezo 4.2 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyepata alama za wastani.

4. Kamilisha nafasi zilizo wazi kwenye barua kwa kuchagua majibu sahihi uliyopewa kwenye kisanduku.

| | | |
|---|---|---|
| Madhumuni | S.L.P 100 | Zawadi |
| 2021 | 13/11/2018 | |

Shule ya Msingi Mwembe,

(i) SLP 100,

Songwe.

(ii) 13/11/2018

Mpendwa mama, shikamoo.

Ni imani yangu kuwa unaendelea vizuri na shughuli za kilimo. Naamini pia ndugu zangu wengine hawajambo hapo nyumbani.

(iii) A ya barua hii ni kutaka kukujulisha kuwa nimefaulu Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne tuliofanya mwishoni mwa mwaka jana. Nimefurahi sana kwa kuwa nimefaulu vizuri kwa kupata Daraja A. Ni matumaini yangu hata mdogo wangu Furaha atafaulu Upimaji wake wa Darasa la Nne wa mwaka (iv) B.

Ninakushukuru kwa kunihimiza kusoma kwa bidii. Kufaulu kwangu kumetokana na maneno yako ya hamasa.

Kwa leo sina mengi zaidi. Ninaomba uwasalimie wadogo zangu wote.


Ni mimi mwanao (v) C.

Kielelezo 4.2: *Jibu la wastani la mwanafunzi katika swali la 4*.

Kielelezo 4.2 kinaonesha sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeweza kujibu kwa usahihi baadhi ya vipengele na kushindwa vipengele vingine kwa kujaza herufi ya jibu kinyume na matakwa ya swali na kupata alama za wastani.

Aidha wanafunzi 433,756 (26.1%) walifaulu kwa kiwango hafifu kati ya alama 0 hadi 2,5 kwani waliweza kujibu kipengele 1 au kushindwa kabisa kutokana na kutokuwa na umahiri wa kubaini vipengele vya muundo wa barua ya kirafiki. Vilevile, wapo wanafunzi ambao walitoa

majibu ambayo ni kinyume na matakwa ya swali, kwa kuandika baadhi ya maneno ambayo hayapo katika kisanduku walichopewa. Vilevile maneno hayo sio lugha sanifu na hayana maana yoyote katika lugha ya Kiswahili. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja aliandika maneno kama vile; *mayahai*, *Zawadi*, *Zamyikasui*, *kuha wasuhi* na *ukahamusyairo*. Maneno hayo yanapatikana katika (i) – (v) kwa mtiririko husika. Hii inathibitisha kuwa mwanafunzi huyo hakuwa na maarifa yoyote kuhusu uandishi wa barua ya kirafiki. Kielelezo 4.3 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi ambaye alijibu vibaya swali.



4. Kamilisha nafasi zilizo wazi kwenye barua kwa kuchagua majibu sahihi uliyopewa kwenye kisanduku.

| | | |
|---|---|---|
| Madhumuni | S.L.P 100 | Zawadi |
| 2021 | 13/11/2018 | |

Shule ya Msingi Mwembe,
(i) mayahai,
Songwe.
(ii) Zawadi

Mpendwa mama, shikamoo.

Ni imani yangu kuwa unaendelea vizuri na shughuli za kilimo. Naamini pia ndugu zangu wengine hawajambo hapo nyumbani.

(iii) Zamyikasui ya barua hii ni kutaka kukujulisha kuwa nimefaulu Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne tuliofanya mwishoni mwa mwaka jana. Nimefurahi sana kwa kuwa nimefaulu vizuri kwa kupata Daraja A. Ni matumaini yangu hata mdogo wangu Furaha atafaulu Upimaji wake wa Darasa la Nne wa mwaka (iv) kuha wasuhi.

Ninakushukuru kwa kunihimiza kusoma kwa bidii. Kufaulu kwangu kumetokana na maneno yako ya hamasa.

Kwa leo sina mengi zaidi. Ninaomba uwasalimie wadogo zangu wote.

Ni mimi mwanao (v) ukahamusyairo.

Kielelezo 4.3: *Jibu baya la mwanafunzi katika swali la 4.*

Kielelezo 4.3 kinaonesha sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeshindwa kukamilisha nafasi zilizo wazi kwenye barua kwa kuandika baadhi ya maneno ambayo hayapo katika kisanduku walichopewa na kupata alama hafifu.

### 2.5 Sehemu E

Sehemu hii ilikuwa na swali moja lenye vipengele vitano (5) vyenye jumla ya alama 10. Swali lilitoka katika umahiri wa kuonesha uelewa wa jambo alilolisikiliza au kulisoma. Swali lilipima ufahamu wa mwanafunzi wa kusoma na kujibu maswali yaliyofuata.

**Swali la 5:** Soma kwa makini shairi lifuatalo kisha jibu maswali yanayofuata kwa **kuandika jibu lililo sahihi** katika nafasi iliyoachwa wazi.

Tusidharau wazazi, heshima kuwafanyia,
Wanafanya kubwa kazi, kutuzaa kutulea,
Wanatupa na mavazi, sisi tunachekelea,
Wazazi wetu ni nguzo, kwetu sisi wana wao.

Wanatutunza vizuri, kwa chakula na mavazi,
Wananunua sukari, chai pia maandazi,
Wanapika na achari, wanatupa na malazi,
Wazazi wetu ni nguzo, kwetu sisi wana wao.

Vilevile zahanati, tunakwenda kutibiwa,
Twaenda kila wakati, ugonjwa tukizidiwa,
Hutupepea kwa dhati, kwa joto tukizidiwa,
Wazazi wetu ni nguzo, kwetu sisi wana wao.

**Maswali**

(i) Shairi hili linahusu nini?

______________________________________

(ii) Neno “malazi” lina maana gani kama lilivyotumika katika ubeti wao?

______________________________________

(iii) Je, mshairi anahitaji watoto wawafanyie nini wazazi wao?

______________________________________


(iv) Katika ubeti wa tatu mshairi anasema kuwa watu wakiugua hupelekwa wapi?

______________________________________

(v) Shairi hili linatoa funzo gani?

______________________________________

Swali hili lilijibiwa na wanafunzi 1,664,019 (100%). Kiwango cha ufaulu katika swali kilikuwa kizuri ambapo jumla ya wanafunzi 131,974 (7.9%) waliweza kujibu vizuri sana vipengele vyote 5 na kupata alama 10. Aidha, wanafunzi 744,080 (44.7%) walifanya vizuri na kupata alama kuanzia 6.5 hadi 9.5. Wanafunzi 614,231 (36.9%) walipata alama za wastani kuanzia 3 hadi 6. Vilevile wanafunzi 510,968 (30.7%) walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 2.5. **Chati Na. 5** inaonesha viwango vya ufaulu wa wanafunzi kwa asilimia.





**Chati Na. 5**: *Asilimia ya ufaulu kwa wanafunzi katika swali la 5*.

Uchambuzi unaonesha kuwa wanafunzi 1,153,051 (69.3%) walikuwa na kiwango kizuri cha ufaulu. Kati yao, wanafunzi 131,974 (7.9%) walifaulu kwa kiwango kizuri sana. Wanafunzi hao waliweza kujibu kwa usahihi vipengele vyote vitano na kupata alama 10 kwa kuwa walikuwa na umahiri wa kusoma shairi na kubaini yaliyomo ndani yake. Kwa mfano, katika kipengele cha (i) kilichomtaka mwanafunzi aeleze shairi linahusu nini, alitoa jibu sahihi kuwa *tusidharau wazazi*. Hii inaonesha kuwa mwanafunzi huyo aliweza kusoma na kuelewa yaliyomo ndani ya shairi.

Vilevile, katika kipengele cha (ii) kilichomtaka mwanafunzi kueleza maana ya neno "malazi" lililotumika katika ubeti wa pili, mwanafunzi huyo alijibu kwa usahihi kuwa ni *sehemu ya kulala.* Hii inaonesha kuwa mwanafunzi huyo licha ya kufahamu yaliyomo kwenye shairi vilevile, aliweza kufahamu ubeti wa pili ni upi kwa kuhusianisha na swali

lilivyoulizwa. Aidha, katika kipengele cha (v) kilichomtaka mwanafunzi kueleza funzo linalopatikana katika shairi, alijjibu kwa usahihi kuwa ni “tuwaheshimu wazazi.” Kwa ujumla, uchambuzi wa majibu ya wanafunzi unaonesha kuwa wanafunzi wengi walikuwa na umahiri wa kusoma na kuchanganua mawazo yaliyowasilishwa katika shairi. Kielelezo 5.1 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeweza kujibu maswali kwa usahihi kutokana na shairi alilolisoma.



5. Soma kwa makini shairi lifuatalo kisha jibu maswali yanayofuata kwa **kuandika jibu lililo sahihi** katika nafasi iliyoachwa wazi.

Tusidharau wazazi, heshima kuwafanyia,
Wanafanya kubwa kazi, kutuzaa kutulea,
Wanatupa na mavazi, sisi tunachekelea,
Wazazi wetu ni nguzo, kwetu sisi wana wao.

Wanatutunza vizuri, kwa chakula na mavazi,
Wananunua sukari, chai pia maandazi,
Wanapika na achari, wanatupa na malazi,
Wazazi wetu ni nguzo, kwetu sisi wana wao.

Vilevile zahanati, tunakwenda kutibiwa,
Twaenda kila wakati, ugonjwa tukizidiwa,
Hutupepea kwa dhati, kwa joto tukizidiwa,
Wazazi wetu ni nguzo, kwetu sisi wana wao.

**Maswali**

(i) Shairi hili linahusu nini?
Tusidharau wazazi

(ii) Neno "malazi" lina maana gani kama lilivyotumika katika ubeti wa pili?
Sehemu ya kulala

(iii) Je, mshairi anahitaji watoto wawafanyie nini wazazi wao?
tuwa heshimu wazazi

(iv) Katika ubeti wa tatu mshairi anasema kuwa watu wakiugua hupelekwa wapi?
Zahanati

(v) Shairi hili linatoa funzo gani?
tuwaheshimu wazazi

Kielelezo. 5.1: *Jibu zuri la mwanafunzi katika swali la 5*.

Kielelezo 5.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyejibu vizuri vipengele vyote vitano kutokana na kuwa na maarifa ya kusoma na kufahamu yaliyomo ndani ya shairi.

Hata hivyo, uchambuzi unaonesha kuwa wanafunzi 614,231 (36.9%) walipata alama za wastani kuanzia 3 hadi 6. Wanafunzi hao waliweza kujibu vipengele 2 hadi 3 vya swali. Aidha, walishindwa kujibu vipengele vingine kwa kukosa umahiri wa kusoma na kubaini yaliyomo katika shairi. Kwa mfano mwanafunzi mmoja alishindwa kujibu kipengele cha (i) kutokana na kutofahamu ujumbe wa shairi husika na katika (ii) alitoa jibu ambalo sio sahihi. Kielelezo 5.2 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeweza kujibu baadhi ya vipengele.

5. Soma kwa makini shairi lifuatalo kisha jibu maswali yanayofuata kwa **kuandika jibu lililo sahihi** katika nafasi iliyoachwa wazi.

Tusidharau wazazi, heshima kuwafanyia,
Wanafanya kubwa kazi, kutuzaa kutulea,
Wanatupa na mavazi, sisi tunachekelea,
Wazazi wetu ni nguzo, kwetu sisi wana wao.

Wanatutunza vizuri, kwa chakula na mavazi,
Wananunua sukari, chai pia maandazi,
Wanapika na achari, wanatupa na malazi,
Wazazi wetu ni nguzo, kwetu sisi wana wao.

Vilevile zahanati, tunakwenda kutibiwa,
Twaenda kila wakati, ugonjwa tukizidiwa,
Hutupepea kwa dhati, kwa joto tukizidiwa,
Wazazi wetu ni nguzo, kwetu sisi wana wao.

**Maswali**

(i) Shairi hili linahusu nini?

(ii) Neno "malazi" lina maana gani kama lilivyotumika katika ubeti wa pili?

Kulea

(iii) Je, mshairi anahitaji watoto wawafanyie nini wazazi wao?

Tusidharau wazazi

(iv) Katika ubeti wa tatu mshairi anasema kuwa watu wakiugua hupelekwa wapi?

Zahanati


(v) Shairi hili linatoa funzo gani?

Tusidharau wazazi
Tuheshimu wazazi

Kielelezo 5.2: *Jibu la wastani la mwanafunzi katika swali la 5*.

Kielelezo 5.2 kinaonesha sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeweza kujibu kwa usahihi baadhi ya vipengele na kushindwa vipengele vingine kwa kukosa umahiri wa kutosha wa kusoma na kubaini yaliyomo katika shairi.

Aidha, uchambuzi zaidi unaonesha kuwa wanafunzi 510,968 (30.7%) walikuwa na kiwango hafifu cha kufaulu. Wanafunzi hao walipata alama kuanzia 0 hadi 2.5 kwakuwa hawakuwa na umahiri wa kusoma na kuwasilisha mawazo yaliyotolewa katika shairi. Kwahiyo walitoa majibu ambayo baadhi yao walinakili kutoka kwenye shairi na mengine walibuni na hayakuwa na uhusianao na matakwa ya shwari. Kielelezo 5.2 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kujibu swali kwa usahihi.



5. Soma kwa makini shairi lifuatalo kisha jibu maswali yanayofuata kwa **kuandika jibu lililo sahihi** katika nafasi iliyoachwa wazi.

Tusidharau wazazi, heshima kuwafanyia,
Wanafanya kubwa kazi, kutuzaa kutulea,
Wanatupa na mavazi, sisi tunachekelea,
Wazazi wetu ni nguzo, kwetu sisi wana wao.

Wanatutunza vizuri, kwa chakula na mavazi,
Wananunua sukari, chai pia maandazi,
Wanapika na achari, wanatupa na malazi,
Wazazi wetu ni nguzo, kwetu sisi wana wao.

Vilevile zahanati, tunakwenda kutibiwa,
Twaenda kila wakati, ugonjwa tukizidiwa,
Hutupepea kwa dhati, kwa joto tukizidiwa,
Wazazi wetu ni nguzo, kwetu sisi wana wao.

**Maswali**

(i) Shairi hili linahusu nini?

chai pia maandazi

(ii) Neno "malazi" lina maana gani kama lilivyotumika katika ubeti wa pili?

tunakwenda kutibiwa

(iii) Je, mshairi anahitaji watoto wawafanyie nini wazazi wao?

kwa chakula na mavazi

(iv) Katika ubeti wa tatu mshairi anasema kuwa watu wakiugua hupelekwa wapi?

hutupea kwa dhati kwa joto

(v) Shairi hili linatoa funzo gani?

tunacheka shairi

maswali wana wao

**Kielelezo 5.3:** *Jibu baya la mwanafunzi katika swali la 5.*

Kielelezo 5.3 kinaonesha majibu ya mwanafunzi aliyejibu vibaya kwa kukosa umahiri wa kusoma na kuwasilisha mawazo yaliyotolewa katika shairi kwa usahihi.

## 3.0 UCHAMBUZI WA KUFAULU KWA WANAFUNZI KATIKA MAHIRI MBALIMBALI

Upimaji wa somo la Kiswahili umehusisha mahiri tano (5) ambazo ni uwezo wa mwanafunzi katika kusikiliza na kuandika matamshi ya silabi, maneno na sentensi (Imla), umahiri wa kubadili majina kuwa vitendo, umahiri wa kutumia lugha ya methali na vitendawili katika mawasiliano mbalimbali, umahiri wa kuunda barua ya kirafiki pamoja na umahiri wa kusoma na kuchanganua mawazo yaliyowasilishwa katika shairi.

Uchambuzi wa viwango vya kufaulu kwa maswali unaonesha kuwa, zipo mahiri zilizokuwa na kiwango kizuri sana, kizuri, na wastani cha kufaulu katika kila swali. Swali la 1, ambalo lilipima umahiri wa mwanafunzi wa kusikiliza matamshi ya silabi, maneno na sentensi (Imla), lilikuwa na asilimia 86.7. Swali la 2 lililopima umahiri wa kubadili majina kuwa vitendo lilikuwa na asilimia 59.9. Swali la 3, ambalo lilipima umahiri wa kutumia lugha ya methali na vitendawili katika mawasiliano mbalimbali lilikuwa na asilimia 69.8. Swali la 4, lilipima umahiri wa kuunda barua ya kirafiki ambapo kiwango cha kufaulu kilikuwa asilimia 73.9 na Swali la 5 lilipima umahiri wa kusoma na kuchanganua mawazo yaliyowasilishwa katika shairi, ambapo lilikuwa na asilimia 69.3 ya kufaulu.

Uchambuzi unabainisha kuwa, swali la 1 lilikuwa na kiwango kizuri zaidi cha kufaulu kwa asilimia 86.7 na swali la 2 lilikuwa na kiwango cha wastani cha kufaulu 59.9% kati ya maswali yote. Hata hivyo, umahiri wa kuwasiliana katika miktadha mbalimbali ndio uliokuwa na alama za juu kwa asilimia 76.8.

## 4.0 HITIMISHO

Uchambuzi wa mahiri mbalimbali unaonesha kuwa, kiwango cha kufaulu kwa mahiri zote katika mwaka 2019 ni kizuri zaidi ya mwaka 2018 ambapo kumekuwa na ongezeko la asilimia 6.0. Mwaka 2019 kiwango cha kufaulu cha wanafunzi katika mahiri kilikuwa asilimia 72.0 ukilinganisha na mwaka 2018 ambapo ni asilimia 66.0.

Uchambuzi huu umebaini changamoto mbalimbali zilizosababisha wanafunzi wasiweze kujibu baadhi ya maswali kwa usahihi. Baadhi ya changamoto hizo ni pamoja na kushindwa kuelewa matakwa ya swali, uwepo wa athari ya lugha mama pamoja na kushindwa kumudu stadi za kusoma na kuandika.

Ili kukabiliana na changamoto za ufundishaji na ujifunzaji ni vema jitihada zifanyike ili kuwawezesha wanafunzi kuwa na weledi wa kumudu somo la Kiswahili ambalo pia ni lugha ya Taifa na ni kielelezo muhimu cha utamaduni wa Mtanzania.

## 5.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

Lugha ya Kiswahili ni lugha muhimu sana katika mawasiliano, ni vema lugha hii ikawekewa misingi madhubuti itakayowezesha ujifunzaji wake kuwa bora. Misingi hiyo inapaswa kuimarishwa kuanzia Shule za Awali hadi Vyuo Vikuu. Mambo yafuatayo yanashauriwa yafanyike ili kuinua kiwango cha ufaulu wa wanafunzi katika Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne:

(a) Walimu watilie mkazo ufundishaji wa kusikiliza na kuandika imla, kama vile;

(i) Kuhakikisha wanafunzi wanaweza kutamka na kuandika sauti za herufi mwambatano mfano *gh, py,*

*pw, sw, nyw* na nyingine katika silabi, maneno na sentensi kwa usahihi kwa kuwapa mazoezi ya mara kwa mara.

(ii) Kuwapa mazoezi ya mara kwa mara ya kutamka na kuandika kwa usahihi maneno yenye herufi ‘s’ na ‘th’ pamoja na ‘z’ na ‘dh’ katika silabi, neno na sentensi.

(b) Walimu watilie mkazo ufundishaji ili kujenga misingi imara ya ujifunzaji, hasa katika kubadili majina kuwa vitendo, kuunda barua ya kirafiki pamoja na kutumia lugha ya methali na vitendawili katika mawasiliano mbalimbali kwa kutumia mbinu za ujifunzaji kama vile;

(i) Mbinu shirikishi

(ii) Mbinu ya bungua bongo

(iii) Kutumia picha mbalimbali

**KIAMBATISHO NA I**

## MUHTASARI WA UCHAMBUZI WA KUFAULU KWA WANAFUNZI KATIKA SOMO LA KISWAHILI KWA KILA UMAHIRI

| Na | **Umahiri Mkuu** | **UPIMAJI WA 2019** | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Kufaulu kwa kila Swali | | Wastaniwa kufaulu | **Maoni** |
| | | **Namba ya Swali** | **% ya kufaulu** | | |
| 1 | Kuwasiliana katika muktadha mbalimbali | 1 | 86.7 | 76.8 | Vizuri |
| | | 3 | 69.8 | | |
| | | 4 | 73.9 | | |
| 2 | Kuonesha uelewa wa jambo alilolisikiliza au kulisoma | 2 | 59.9 | 64.6 | Vizuri |
| | | 5 | 69.3 | | |

**KIAMBATISHO NA 2**

## ULINGANIFU WA KUFAULU KWA WANAFUNZI KWA KILA UMAHIRI KATIKA SFNA 2018 NA SFNA 2019

| Na | Umahiri Mkuu | Mtihani wa Upimaji 2018 | | | | Mtihani wa Upimaji 2019 | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kufaulu kwa kila Swali | | Wastani wa ufaulu (%) | Maoni | Kufaulu kwa kila Swali | | Wastani wa ufaulu (%) | Maoni |
| | | Namba ya swali | (%) ya ufaulu | | | Namba ya swali | (%) ya ufaulu | | |
| 1. | Kuonesha uelewa wa jambo alilolisikiliza au kulisoma | 5 | 76.8 | 76.8 | Vizuri | 2 | 59.9 | 64.6 | vizuri |
| | | | | | | 5 | 69.3 | | |
| 2. | Kuwasiliana katika miktadha mbalimbali | 1 | 90.3 | 63.2 | Vizuri | 1 | 86.7 | 76.8 | vizuri |
| | | 2 | 80.8 | | | 3 | 69.8 | | |
| | | 3 | 39.6 | | | 4 | 73.9 | | |
| | | 4 | 42.1 | | | | | | |